Mwananch Uk. 22, Tarehe 06/10/2020

Uvuvi ulivyochambuliwa katika ilani za vyama

CUF

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo ili kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya uvuvi nchini:

- Itaanzisha mfuko rasmi wa kuhamu wa mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi na wananchi wengine wenye nia ya kujajiri kwenye sekta hiyo kwa ajili ya kumsaidia vifaa vya kisasa vya uvuvi na hifadhi, na kuanzisha ufugaji wa samaki (fish farming).
- Itatoa huduma ya mafunzo kwa wavuvi kwa kiasi kikubwa yatakayolenga katika matumizi ya njia bora za hifadhi ili kuhakikisha kuwa mavuno ya wavuvi hayapotezi ubora wake kabla ya kufikia kwenye soko.
- Itaimarisha shughuli za doria katika maeneo ya uvuvi ili kuhakikisha kuwa wavuvi hawaendelei na utaratibu wa uvuvi unaoharibu mazingira na kuleta maangamizi makubwa kwa samaki na viumbe wengine wa majini, ambao una mueleko wa kuhatarisha ajira kwenye sekta ya uvuvi.
- Itaweka utaratibu wa kisheria unaohitaji wasindikaji wa mazao ya samaki kununua samaki kiasi maalum cha samaki kila wanaponunua, kutoka kwa wavuvi wadogo wadogo. Utaratibu huu utasaidia uwepo wa mzunguko wa fedha kwa kutoa ajira kwa wananchi wetu.

NCCR MAGEUZI

Kuhamasisha na kuhakikisha wananchi wanachukua fursa ya ufugaji wa samaki kwa njia za kisasa kwa kushirikiana na vyuo vya uvuvi na ufugaji samaki vya Mbegani na Nyegezi.

- Kupunguza au kufuta kodi ya ungizaji wa chakula cha samaki kutoka nje ya nchi
- Kupunguza masharti ya ufugaji wa samaki wa vizimba kwa kuruhusiwa wananchi kupata vibali kwa wakati na katika kituo kimoja cha kutolea huduma.
- Kuhamasisha wananchi kutumia fursa ya kulima mazao ya bahari kama majongoo bahari na mwani na kuongeza thamani ya mazao hayo
- Kuhalalisha mialo iliyopo na kuongeza idadi ya mialo katika pwani ya bahari ya Hindi na maziwa. Kuongeza na kuimarisha maeneo ya uuzaji ya samaki kwa kuimarisha miundombinu ya masoko hayo.
- Kumuunua meli za uvuvi angalau saba zenye uwezo wa kuvua samaki bahari kuu.
- Kujenga bandari ya uvuvi katika ukanda wa Pwani ambayo itawezesha meli zinazovua Bahari Kuu kutia nanga.
- Kurejesha mazalia na makazi ya samaki yaliyoharibika kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa kuweka matumbawe bandia na kupanda mikoko katika bahari.
- Kushirikiana na Mashirika ya Umma yenye dhamana ya uvuvi nchini, kuwavutia wawekezaji kuanzisha viwanda vya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi, vyombo na zana za uvuvi.
- Kuboresha maeneo ya uvuvi kwa kutumia teknolojia rafiki ya mazingira kwa kuweka vifaa vya kuvutia samaki baharini ili kuwawezesha wavuvi wadogo kuyafikia maeneo yenye samaki wengi na hivyo kuongeza upatikanaji wa samaki.
- Kuendeleza utafiti wa kurudishia samaki na kupandikiza samaki ili kuongeza wingi katika maziwa, mito na mabwawa.
- Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji wa samaki kwa lengo la kukuza ufugaji wa samaki nchini.
- Kushirikiana na wadau wa ufugaji samaki ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kujenga mabwawa ya kufugia samaki na kuongeza uzalishaji ili kupanua wigo wa ajira kwa vijana.



18
Idadi ya maeneo tangulie yatakayoimarishwa na CCM

20%
Kiwango cha bajeti cha ACT kwenye sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi

ACT WAZALENDO

Itawekeza na kuhakikisha uvuvi na ufugaji endelevu unafanyika kote nchini, ikiwemo kuwekeza katika minada ya kisasa na kupanua soko la bidhaa za ufugaji na uvuvi ndani na nje ya nchi.

- Itaboresha mazingira ya kufanya biashara kwa mazao ya majini kama mwani, ili kuwanufaisha wavuvi nchini.
- Itatenga 20% ya bajeti ya maendeleo kwenye Sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, mara mbili zaidi ya makubaliano yaliyozimiwa na Umoja wa Afrika(CAADAP).
- Kuwezesha uwekezaji kwenye bandari za uvuvi ili kuimarisha uvuvi bahari kuu kufikia lengo la mazao nje ya mapato ya uvuvi yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.

CCM

Itajenga bandari ya uvuvi katika ukanda wa Pwani ambayo itawezesha meli zinazovua kutia nanga kwa lengo la kuhamasisha na kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na huduma nyingine. Katika hatua hii inatarajiwa kuzalisha takribani ajira 30,000 na kuongeza pato kwa jami.

- Itaweka mazingira bora katika uvuvi wa bahari kuu kwa kutoa viyuio kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kwa kutekeleza kikamilifu Sheria ya kusimamia na kuendeleza Uvuvi wa Bahari kuu ya mwaka 2020.
- Itaburi na kutekeleza mikakati ya kuwaelimisha wavuvi juu ya matumizi ya zana bora na kushirikiana na wananchi katika matumbano dhidi ya uvuvi haramu ili kuwa na uvuvi endelevu na wenye tija kwa vizazi vya sasa na vijavyo.
- Itaimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo tisa katika maeneo ya Ziwa Victoria (3), Ziwa Tanganyika (4) na Ziwa Nyasa (2).
- Vilevile, itaimarisha masoko ya samaki ya Feri (Dar es Salaam), Kirumba (Mwanza), Kipumbwi (Pangani), Sahare (Tanga) ili kuongeza thamani na ubora wa samaki pamoja na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi.
- Itaimarisha teknolojia rahisi za uzalishaji, uhifadhi na uchakataji wa samaki kwa kujenga mitambo ya kuzalisha barafu, mitambo ya kukausha samaki hususan dagaa na vyumba vya baridi vya kuhifadhi samaki katika maeneo ya uvuvi ili kuimarisha mnyororo wa thamani.
- Itaanzisha maeneo mapya ita ya hifadhi katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na kuimarisha hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu 18 ili kuhakikisha kuwa mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika yanarejeshwa katika hali yake ya awali.
- Itarejesha mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa kuweka matumbawe bandia na kupanda mikoko katika bahari ili kuongeza wingi wa samaki.
- Itahamasisha uanzishaji na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya msingi vya wavuvi wadogo kwa lengo la kuwapatia mitaji, ujuzi na vifaa pamoja na zana za uvuvi katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi, maziwa, mabwawa na mito ili kuongeza uzalishaji, ajira na kipato.

CHADEMA

Serikali ya Chadema itaanzisha mchakato wa kuridhia Mkataba wa kazi za Uvuvi (The Work in Fishing Convention, 2007 - No. 188), Port State Measure Agreement (PSMA) na UN Fish stock Agreement

- Itaimarisha ushirikiano na Taasisi za uvuvi za kikanda na zile zilizopo katika bahari ya hindi magharibi (Western Indian Ocean-WIO) ili kuweza kuhadilishana taarifa kuhusiana na mambo mbali mbali ikiwemo uvuvi haramu(IUU fishing) na samaki wanaohama-hama kama samaki aina ya jodari (Tuna)na aina yake kwa Ukanda wetu wa EEZ.
- Serikali ya Chadema itapitia na kuandaa Mkakati wa Kufuatilia, kudhibiti na kuchunguza (Monitoring control and surveillance -MCS) na itifaki zinazokwenda sambamba na sheria za kimataifa na kikanda juu ya uvuvi haramu wa bahari kuu.
- Itaandaa Mpango Kazi utakaoruhusu usajili wa meli za uvuvi za kimataifa kwa kutumia mfumo maalum wa utambuzi wa meli (Unique Vessel Identifier – 65 UVI) kupitia IMO. Mamlaka za Uvuvi kwa kushirikiana na Mamlaka za Usafiri wa bahari zitaandaa mfumo huu na itifaki husika au Hati ya makubaliano (MoU).
- Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itazunua Boti kubwa ya kisasa itakayoweza kufanya kazi za doria na utafiti kwenye ukanda wote wa bahari kuu ili kukabiliana na ujangili wa Meli za nje kuvua na kuipotezea serikali mapato yake.

Scanned with CamScanner

*Black Australorp: Kuku anayeweza kufugwa kisasa, kienyeji

Mtanzania Uk. 13, Tarehe 06/10/2020

Inatoka uk. i

nchini, na ni wazuri pia kwa ufugaji huria, kwa kuwachia nje wajitafutie chakula wenyewe.

Kuku huyo ana sifa ya kuweza kumpatia mfugaji faida kupitia mayai na nyama ni wazuri kwa biashara za mazao yote mawili.

Ingawa wanajulikana kwa sifa zao ya utagaji mayai mengi, lakini kuku huwa wanafaa kwa nyama pia, kwani huwa na nyama nyingi sana (dual purpose chickens).

Utagaji wao wa mayai unakaribia ule wa kuku wa kizungu, huanza kutaga wakiwa na umri wa miezi mitano na nusu hadi sita.

Kwa wastani Black Australorp, hutikisha mayai 250 kwa mwaka, wakiwa katika mazingira mazuri.

Hawana sifa nzuri ya kulalia mayai, lakini akilalia hutotoa vifaranga vingi, na ni wazuri kwa uleaji wa vifaranga hivyo.

Kuku hawa ni wakubwa, wazito, na endapo mfugaji akiwalisha vizuri jogoo anaweza kufikisha uzito wa kilogramu 3.5 hadi tano na kwa tetea hadi hufikisha kilogramu tatu hadi 3.7.

Pia nyama ya kuku hao inaelezwa kuwa na ladha tamu.

Black Australorp ni wagumu, hawapati magonjwa mara kwa mara, hivyo basi huvumilia magonjwa ya aina nyingi na hawachagui chakula. Wanakula vyakula wanavyokula kuku wengine wa kienyeji.

Kuku hawa ni wapole na rafiki kwa binadamu na wanamvuto sana kuwaangalia hivyo wakati mwingine huwa kama mapambo katika nyumba.

Wana michirizi ya kijani pale wanapomulikwa kwenye mwangi mkali wa jua, wanapendeza pia kwa ufugaji mdogo, katika mazingira ya nyumbani.

Australorp ni asili ya kuku wa Australia alianza kufahamika ulimwenguni kote katika miaka ya 1920 baada ya kuzaliana na kuvunja rekodi nyingi za dunia kwa idadi ya mayai.

Huyu ni kuku anaeheshimika ndani ya Taifa la Australia, rangi maarufu zaidi ya kuku huyu ni mweusi, lakini kuna bluu na nyeupe pia.

Asili ya jamii hii ya kuku ni Australia kutoka Black Orpingtons wakitokea Uingereza kwa lengo la kueneza uzalishaji wa mayai kwa wingi na nyama.

Asili ya jina Australorp kwa mara ya kwanza kabisa lilitolewa na moja ya taasisi za pembejeo za mifugo hasa kuku chini ya William Wallace Scott, kabla ya Vita Kuu ya Kwanza.

Kutoka 1925 Wal Scott alianza kufanya kazi ili kumtambulisha Australorp kuwa ni ndiye kuku anayezalisha zaidi na huyo ndio kuku wa Malawi.

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk. 9, Tarehe
06/10/2020

Wafugaji watakiwa kuwatumia wataalamu

Na Futuma Selemani, KIBAHA

SERIKALI imewataka wafugaji wajenge tabia ya kuwashirikisha na kuwatumia wataalamu wa mifugo kujua chanzo sahihi cha magonjwa yanayoikabili mifugo yao badala ya kujigeuza wao madaktari wa mifugo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Prof. Elisante ole Gabriel, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea Taaasisi ya Chanjo Kibaha na kutembelea kiwanda cha kutengeneza chanjo za mifugo kilicho chini ya wizaya hiyo kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kisha kuzungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari waliotembelea kuona shughuli zinazofanywa na taasisi hiyo inayoendeshwa na wakala hiyo.

"Kuna baadhi ya wafugaji wanadhani kuwa ng'ombe ni wao, wanadhani wanaweza kuwa madaktari mara nyingine hata mtu akiwa na zahanati yake lazima amshirikishe daktari ajue anatibiwa vipi, ingawa jengo ni la kwake, hawezi kusema nipeni dawa hii ile na ile hapana," alisema Prof. Gabriel na kuongeza:

"Hoja yangu wafugaji lazima wawatumie wataalamu wa mifugo waambiwe chanzo sahihi kinachoikabili mifugo yao kwa kudhani ukimchoma ng'ombe sindano ya DT'T ndio unahisi vidudu vyote vya sotoka vitakufa hapana."

"Watanzania wapate chanjo kwa bei rahisi, wafugaji wafuge kisasa na kutoa tiba nzuri kwa mifugo...Watanzania nunueni chanjo zilizohakikiwa katika ubora unaotambulika kwa bei inayostahili," alisema.

Aidha, alizishauri halmashauri kutoa kipaumbele katika sekta ya mifugo kwa mujibu wa sheria, na kuelekeza kuwa asilimia 15 itokanayo na mapato ya ndani kutokana sekta ya mifugo irudi kuendeleza sekta hiyo.

"Lengo ni ndani ya halmashauri kuwapo na mkakati wa kuendeleza mifugo kwa kutumia chanjo zilizoratibiwa kufuatia idhibati TVLA inazalisha chanjo hizo ni muhimu zitumike kwa usalama wa wanyama na kulinda afya za watu," alisema.

Aliwataka wataalamu wa mifugo watambue hawapo kwa maslahi yao binafsi bali ni kuwasaidia wafugaji ili wawakumbuke kwa mchango wao.

"Kila mtu atoe mchango wake kitaalamu kusaidia wafugaji, lazima ukiondoka watu wakukumbuke michango yenu sio vyeo vyenu, mnajua chanjo ipi imsaidie mfugaji," alisema.

Alisema kituo kinasaidia mno chanjo katika matibabu ya mifugo, hivyo ni muhimu Watanzania waelewe chanjo huchanjwa ng'ombe au mifugo kabla haijaugua na hufanyika kwa wingi, hivyo ikipelekwa chanjo ambayo sio yenyewe italeta madhara makubwa kwa taifa.

Katika hatua nyingine, Prof. Gabriel alisema wizara imeanza mazungumzo na Shirika la Bima la Taifa (NIC) kwa ajili ya uanzishwaji wa bima ya mifugo.

Alisema wameshazungumza na Mkurugenzi Mkuu wa NIC, Dk. Elirehema Doriye na kwamba mazungumzo yanakwenda vizuri.

Scanned with CamScanner

Wadau sekta ya mifugo kupatiwa huduma bora

Na Mwandishi Wetu, Kibaha

WAKALA ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imejipanga kuwahudumia wadau katika sekta ya mifugo kwa kuwapatia huduma bora za uchunguzi na utambuzi wa magonjwa, kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo na kupima nguvu ya dawa za kuogeshea mifugo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dkt. Furaha Mramba, wakati akizungumza na wahahari wa vyombo mbalimbali vya nchini waliotembelea Taasisi ya Chanjo Kibaha (TVI) iliyopo Kibaha, mkoani pwani.

Pia alisema wamejipanga kutengeneza na kuwasambazia wafugaji chanjo za mifugo na wadau wengine na hivyo alitoa wito kwa wananchi kufika TVLA kwa ajili ya kuhuduniwa.

Kwa mujibu wa Dkt. Furaha Taasisi ilianzishwa ili nchi iweze kuzalisha chanjo zote muhimu zitakazokidhi mahitaji ya idadi kubwa ya mifugo kwa bei ya chini na kuiondolea Serikali mzigo wa kuagiza chanjo nje ya nchi.

Alisema taasisi hiyo hadi sasa imefanyakazi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Kwa mujibu wa Dkt. Mramba Taasisi hiyo ina vitengo vikuu viwili, ambavyo ni Kitengo cha Chanjo za virusi ambacho kinazalisha chanjo aina ya Mdondo stahimilivu joto inayofaa zaidi kwa kuku wa kienyeji.

"Chanjo huu imefanya vizuri sana katika maeneo wanayochanja ambapo mdondo umedhibitiwa kwa asilimia 95 kwa wale wanaofuata ratiba ya uchanjaji ya mara tatu kwa mwaka," alisema Dkt. Mramba.

Kwa upande wa uzalishaji wa Chanjo za Bakteria, Dkt. Mramba alisema wanazalisha chanjo aina nne kwa sasa. Alitaja chanjo hizo kuwa ni za Kimeta, Chambavu, Kutupa Mimba na Mapafu ya Ng'ombe.

Akifafanua zaidi kuhusu chanjo ya mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu (TECOBLAX), Dkt. Mramba alisema chanjo hizo huhakikiwa na Maabara ya Chanjo za Veterinari ya Umoja wa Afrika (AU-PANVAC iliyoko Ethiopia) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)

Alisema Chanjo ambazo ziko kwenye hatua mbali mbali za utengenezaji ni pamoja na chanjo ya mapafu ya mbuzi, Sotoka ya mbuzi na mondoo na kichaa cha mbwa.

Alitaha chanjo zingine zinazotegemewa kuzalishwa kadri rasilimali fedha inavyopatikana kwa mujibu wa Dkt. Mramba ni Ndigana Kali, Miguu na Midomo, Mapele Ngozi na Bonde la Ufa.

Kwa upande wa changamoto, alisema wanakabiliwa na upungufu wa majengo ya kuzalishia chanjo, kiwanda kina jengo moja la kuzalishia chanjo na sasa kuna ujenzi wa jengo unaoendelea ambapo likikamilika litatumika kuzalisha chanjo za bakteria za sasa na mpya zilizoko kwenye majaribio na zingine ambazo ziko kwenye mpango wa kuzalishwa ili kufikia chanjo aina 13 kulingana na mpango mkakati wa wizara

Nyingine ni ukosefu wa miundombinu ya usambazaji wa chanjo, Wakala unahitaji magari maalumu (Refrigerated Trucks) angalau matano pia magari kwa ajili ya vituo vyote 12 ambavyo kwa sasa vina magari chakavu kabisa yenye umri wa zaidi ya miaka 15.

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk. 10, Tarehe
06/10/2020



Scanned with CamScanner

The Guardian Uk. 5, Tarehe
06/10/2020

Mafia Island Marine Park's whaleshark population up

By Guardian Reporter

THE population of whale sharks in Mafia Island Marine Park has increased to 206 in December 2019 from about 100 in 2012, according to a report published by the WWF Tanzania.

The report said the increase followed an effective conservation jointly implemented by WWF and the government of Tanzania.

Since early 2012 WWF facilitated awareness raising to the stakeholders, including fishers, boat riders, tour operators, tour guides, district authorities, hoteliers and other investors on the importance of coordinated management of whale sharks on Mafia Island Marine Park, said the report published in WWF Tanzania's Conservation Bulletin.

The report said threats that put whale sharks at risk included entanglement in fishing nets, injuries caused by boat rides and hunting for meat and fins.

"Even if fishers are not trying to catch the sharks, but their large ring-nets can trap, entangle and injure the whale sharks. Sharks can get amputated especially the fins during untangling from fishing nets," said the report.

Mafia Island, located 20 kilometers offshore from the eastern extent of the Rufiji delta on the southern coast of Tanzania, is the only home for the whale sharks in the country.

Whale sharks are protected and listed in the International Union for Conservation of Nature red list of endangered, threatened and protected species.

Scanned with CamScanner

Bashungwa akagua ujenzi wa kiwanda cha maziwa

Na Mwandishi Wetu

■■ WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa amemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Profesa Riziki Shemdoe kufika kwenye kiwanda cha maziwa kinachojengwa Kharga, Karagwe ili kutatua changamoto anazokipata mwekezaji wa kiwanda hicho.

Bashungwa alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua ujenzi wa kiwanda cha kuchakata maziwa cha Kahama Fresh, kinachojengwa eneo maalumu la viwanda lilopo Kharga wilayani Karagwe Mkoa Kagera.

Waziri huyo alipongeza jitihada za mwekezaji mzawa wa Kahama Fresh Limited, Jossam Mtangeki kwa kusaidia utekelezaji wa dira Serikali ya awamu ya tano katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuwa mkoa ulikuwa na kiwanda cha maziwa chenye ukubwa wa kuchakata lita 10,000 kwa siku.

Alifurahishwa na mpango wa uwekezaji ambapo kutakuwa na kiwanda kinachotengeneza vyakula vya ng'ombe wa maziwa, pia alipongeza kwa kuwepo kwa shamba la ngo'ombe wa mfano ambalo linawasaidia wafugaji wadogo wadogo kupata elimu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Waziri Bashungwa aliyadiliana na mwekezaji huyo mpango wa kugawa ngo'ombe kwa wafugaji wadogo wadogo na namna ya kuwasaidia wafugaji hao, ili kupitia serikali, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo ziweze kuwaweka hao wafugaji wadogo katika mfumo wa ushirika.

Nayo Mkurugenzi wa Kahama Fresh Limited, Jossam Mtangeki alieshukuru serikali kupitia Waziri Bashungwa kwa kuendelea kuweweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kutenga maeneo maalumu ya viwanda kwa kila wilaya na kuwasogezea mahitaji muhimu ambayo yanahitajika katika uwekezaji wao.

Jossam wakati akitoa taarifa ya kiwanda kwa Waziri Bashungwa, alisema ujenzi wa kiwanda hicho umefikia kiwango cha kujenga majengo ya ofisi na kusanzisha eneo kitakapojengwa kiwanda ambacho kitakamilika ndani ya miezi sita na kitakuwa na uwezo wa kuchakata lita 10,000 kwa muzunguko mmoja na gharama za ujezi mpaka kukamilika ni sh. bilioni 2.4.

Alitoa wito kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, kuitumia fursa hiyo ya kiwanda hicho kukabiliana na changamoto ya soko la mazwa, ambalo likuwa ni tatizo la muda mrefu ambapo alwaombe wafugaji wa Mkoa kagera, kujikita na kuendelea kufuga ng'ombe wa maziwa kwa tija ambao utasaidia kiwanda hicho kufanya kazi, pia na wao kunufaika kupitia uwepo wa soko la uhakika la maziwa.

Scanned with CamScanner

Tanzania yazalisha chanjo sita za mifugo

Na Mwandishi Wetu, Kibaha

TANZANIA imepiga hatua kubwa katika uzalishaji wa chanjo za mifugo baada ya kuzalisha chanjo sita katika muda mfupi.

Aidha, chanjo ya saba inatarajiwa kufanyiwa majaribio hivi karibuni baada ya kuwa majaribio ya awali yakiwa yameanza.

Hayo yamefahamika mwishoni mwa wiki mjini hapa wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Profesa Elisante ole Gabriel pamoja na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini katika taasisi mbili zinazohusika na chanjo za mifugo.

Taasisi hizo ni Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) na Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI).

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk Furaha Mramba, tangu uzalishaji wa chanjo uanze rasmi mwaka 2014, wameshatengeneza chanjo sita.

Dk Mramba alisema TVI ilianza kwa kuzalisha chanjo moja tu dhidi ya ugonjwa wa mdondo wa kuku yenye jina la kibiashara la TEMEVAC.

Lakini alisema hadi kufikia mwaka huu, wanazalisha chanjo aina sita ambazo ni chanjo dhidi ya ugonjwa wa Mdondo kwa kuku; ya Kimeta kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo; ya Chambavu kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo, ya Kutupa Mimba kwa ng'ombe, na chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe kwa ajili ya ng'ombe.

Aliitaja ya sita kuwa ni ya mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu ya kukinga magonjwa hayo mawili kwa mara moja.

"Lengo la karibuni la wakala ni kupanua wigo wa aina za chanjo zinazozalishwa kwa kuongeza chanjo tatu za kimkakati," alisema Dk Mramba na kuzitaja chanjo hizo tatu ni ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP), Sotoka ya mbuzi (PPR) na Kichaa cha Mbwa (Rabies).

Kuhusu Homa ya Mapafu ya Mbuzi, alisema, "Majaribio ya awali ya chanjo dhidi ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi tayari yameshaanza na inategemewa kuwa ifikapo Desemba 2020 chanjo hii itakuwa tayari inafanyiwa majaribio katika baadhi ya maeneo."

Alisema kwa majaribio ya chanjo ya Sotoka ya mbuzi yanategemewa kuanza baada ya watumishi kupata mafunzo maalumu juu ya uzalishaji huo.

Dk Mramba alisema kwa ile ya Kichaa cha Mbwa majaribio ya utengenezaji wa Mbegu Kuu kutokana na vimelea vya virusi vya ugonjwa huo yanaendelea kufanywa na maabara ya CIDB.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga alisema kuna magonjwa 13 ya kimkakati ambayo Tanzania inataka kuyadhibiti ili kuleta tija katika mifugo nchini.

Dk Nonga aliyataja kuwa ni homa ya mapafu ya ng'ombe, homa ya mapafu ya mbuzi, midomo na miguu, mapele ngozi, kutupa mimba, sotoka ya mbuzi na kondoo na ndigana kali, mdondo, kichaa cha mbwa, homa ya Bonde la Ufa, homa kali ya nguruwe na chambavu.

Alisema nia ya serikali ni kuhakikisha magonjwa hayo yanapata chanjo ili yatokee kabisa kama ilivyo kwa chanjo ya mdondo wa kuku ambayo imeleta mafanikio kwa kudhibiti ugonjwa huo nchini kwa asilimia 95 kwa wafugaji.

Meneja wa Taasisi ya Chanjo Tanzania, Dk Stella Bitanyi alisema kinazalisha dozi milioni 60 kwa mwaka kulingana na mahitaji, ingawa wanaweza kuongeza hadi kufikia milioni 100.

Dk Bitanyi alisema endapo watapatiwa vifaa zaidi wataweza kuzalisha zaidi na hata kuuza nje chanjo kwani chanjo zao zina ubora wa juu kiasi kuwa katika maeneo ya mipakani imegundulika chanjo ya mdondo inavushwa nchi za jirani za Malawi, Burundi na Kenya.

Katibu Mkuu Mifugo, Profesa Ole Gabriel alisema uzalishaji wa chanjo hapo nchini una faida tatu kubwa.

Alizitaja kuwa ni usalama wa nchi hasa kutokana na kuwapo kwa uhusiano mkubwa kati ya afya ya binadamu na ya mifugo, usalama wa afya ya watu na usalama wa afya ya mifugo.

Aliwataka wafugaji kutumia chanjo zinazozalishwa na TVI kwani zina ubora na zinapatikana kwa gharama nafuu.

Tanzania ni nchi ya pili kwa mifugo mingi barani Afrika baada ya Ethiopia, ikiwa na ng'ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.9, kondoo milioni 5.7, kuku milioni 83.3, nguruwe milioni 2.2 na punda 660,000.

Sekta ya mifugo inakua kwa asilimia saba na inachangia Pato la Taifa kwa asilimia 7.6. Mwaka 2016 mapato ya sekta ya mifugo yalikuwa Sh bilioni 14.1, lakini mwaka huu yamefikia Sh bilioni 44.8 sawa na ongezeko la asilimia 210.

Scanned with CamScanner

Habari Leo Uk. 19, Tarehe 06/10/2020

Chwaka wapewa boti za kisasa za uvuvi

WANANCHI wa Jimbo la Chwaka lenye vijiji sita, wameahidiwa kupewa boti za kisasa za uvuvi, zitakazowawezesha kuvua kwenye maji yenye kina kirefu na kupata mapato mengi ya samaki.

Hayo yamesemwa na Mgombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chaumma, Ali Omar Juma wakati akihutubia mkutano wa kampeni katika Jimbo la Chwaka Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema wavuvi katika jimbo hilo, wanashindwa kupata kipato kikubwa cha samaki kutokana na kushindwa kuvua katika kina kikubwa cha maji.

"Nikichaguliwa kuwa rais nataka niwapatie wananchi wa Jimbo la Chwaka lenye jumla ya vijiji sita boti za kisasa zitakazowawezesha kuvua samaki na kuvuna rasilimali nyingi za baharini," alisema.

Mapema Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Faki Saluni Abdalla alisema wanatarajia kujenga kiwanda cha kusindika ndimu, ambazo zinazalishwa kwa wingi na wakulima wa kijiji hicho.

Scanned with CamScanner